

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA KUHITIMU KIDATO CHA SITA**

121/2

KISWAHILI 2

(Kwa watahiniwa Walioko Shuleni na Wasiokuwa Shuleni)

Muda: Saa 3

Mwaka: 2020

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali **nane (8)**.
2. Jibu maswali yote katika sehemu A na maswali **matatu (3)** kutoka sehemu B.
3. Sehemu A in alama **arobaini (40)** na sehemu B ina alama **sitini (60)**.
4. Zingatia maagizo ya **kila sehemu** na ya **kila swali**.
5. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org



SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Uhuru wa mwandishi ni zao bora la kazi ya fasihi. Eleza hoja hiyo ukionesha vipingamizi vitano (5) vinavyoingilia uhuru wa mwandishi na kusababisha kazi zake kupwaya.
2. Hadithi na sanaa za maonesho ni tanzu za fasihi simulizi zenye kufanana na kutofautiana. Fafanua kwa ufupi usemi huo kwa kutoa hoja tatu za kufanana na hoja mbili za kutofautiana kwa tanzu hizo.
3. Kwa kutumia hoja tano, eleza sifa za mtambaji wa fasihi simulizi.
4. Fafanua kwa kutoa mifano dhahiri vipengele vya kisanaa vilivyotumika katika shairi lifuatalo:

Napiga mbiu Nianga, namwambisha wafugao,
Wafuge na kuwafunga, ng'ombe wapate mazao,
Kwa wema mkiwafuga, watawapatia fao,
Ng'ombe asiyemchungu, hakosi kutangatanga.

Ng'ombe mazizini mwao, wengi wanaowafunga,
Na usumbufu wanao, matilaba kuwapanga,
Na kuwaweka kikao, kwa kukosa kuwachunga,
Ng'ombe asiyemchungu, hakosi kutangatanga.

Dawa ya ng'ombe mchungu, mchungu ndo dawa yao,
Vipodozi kuwakinga, wasipoteze mazao,
Mjinga asiyeiga, kwa wenzie wafugao,
Ng'ombe asiyemchungu hakosi kutangatanga.

Wapeni mikomamanga, ing'aze miili yao,
Na muwe mkiwachunga, kwa sifa ziwapasao,
Kwa wema mkiwachunga, watawapatia fao,
Ng'ombe asiyemchungu, hakosi kutangatanga.

Nimefikia kituo, tamati natia nanga,
Wapeni maangalio, naomba mnaofuga,
Sasa watoto ninao, wangu mie namchungu,
Ng'ombe asiyemchungu, hakosi kutangatanga.

SEHEMU B (Alama 60)

Jibu maswali **matatu (3)** kutoka sehemu hii. Swali la **tano (5)** ni la lazima.

ORODHA YA VITABU KWA SWALI LA 5-8

USHAIRI

Kimbunga	-	Haji Gora
Mapenzi Bora	-	Shabani Robert
Chungu Tamu	-	Theobald A. Mvungi
Fungate ya Uhuru	-	Mohamed S. Khatibu

RIWAYA

Usiku utakapokwisha	-	Mbunda Msokile
Kufikirika	-	Shabani Robert
Mfadhili	-	Hussein Tuwa
Vuta N'kuvute	-	Shafi Adamu Shafi

TAMTHILIYA

Kwenye Ukingo wa Thim	-	Ebrahim Hussein
Morani	-	Emmanuel Mbogo
Kivuli Kinaishi	-	Said Mohamed
Nguzo Mama	-	Penina Muhando

5. Bainisha mafunzo yanayotolewa na washairi kwa jamii kwa kutoa hoja nne kwa kila kitabu kutoka katika diwani mbili ulizosoma.
6. Kwa kutumia hoja tatu kwa kila diwani, eleza umuhimu wa kipengele cha lugha kwa mtunzi wa shairi ili kumwezesha msomaji kupata ujumbe uliokusudiwa katika diwani mbili ulizosoma.
7. “Mwandishi wa fasihi ni chachu ya mabadiliko chanya katika jamii ili kuwa na maisha bora.” Thibitisha kauli hiyo kwa kutumia riwaya mbili ulizosoma. Toa hoja nne kwa kila kitabu.
8. “Fasihi andishi ya Kiswahili ni kapu kubwa lililosheheni semi.” Thibitisha hoja hiyo ukitumia misemo mitatu, methali tatu na nahau tatu kwa kila kitabu katika tamthiliya mibili ulizosoma, kisha onesho lengo la mwandishi katika kutumia semi hizo.